

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO
{Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)}

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**S.L.P. 43,
KIBONDO.**



Simu Na. 028-2820084
Fax Na. 028-2820270
Unapojibu tafadhali taja:
HW/H/PMU/18/19/V.3

Tarehe. 01/02/2019

**TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI WA JENGO LA KIBODECO HOTEL KWA
KIPINDI CHA KUENZIA 1. MACHI 2019 HADI 28. FEBRUARI, 2020**

Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo inakaribisha maombi kutoka kwa Taasisi/Kampuni/Vikundi/watu binafsi wenye nia ya kuingia ubia na Halmashauri ya wilaya ya Kibondo kuendesha Hotel ya Kibodeco iliyoko Wilayani Kibondo.

MASHARTI YA KUOMBA UZABUNI.

- (a) Mwombaji akiwa mtu binafsi awe ni raia wa Tanzania mwenye sifa, kama ni kikundi, Tasisi isiyo ya kiserikali au Kampuni iwe imesajiliwa kisheria.
- (b) Mwombaji aambatishe pamoja na maombi yake nyaraka zifuatazo:
 - Kivuli cha leseni ya biashara yoyote.
 - Kivuli cha cheti cha usajili wa mlipa kodi TIN.
 - Kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi.
- (c) Ada ya maombi ni Tsh 50,000.00 ambayo **haitarudishwa** na italipwa na kupokelewa na karani wa fedha katika ofisi ya Mweka Hazina na kukatiwa stakabadhi.
- (d) Mwombaji aliyeshinda zabuni atalipa dhamana ya Mkataba ikiwa ni sawa na kiwango cha miezi mitatu wakati wa kufunga Mkataba kabla hajaanza kukusanya.
- (e) Maombi yote yatatumia nyaraka za zabuni zinazopatikana kwenye ofisi ya Katibu wa bodi ya zabuni baada ya kulipia ada ya maombi.
- (f) Maombi yafungwe vizuri kwenye bahasha na juu yake iandikwe utambulisho wa zabuni na kutumwa kwa anuani ifuatayo:

KATIBU WA BODI YA ZABUNI

HALMASHAURI YA WILAYA KIBONDO,


**S.L.P. 43,
KIBONDO**

Kwa njia ya Posta au kwa kupelekwa kwa mkono na kutumbukizwa kwenye sanduku la Zabuni lililoko katika Ofisi ya Ununuzi na Ugavi (W) Idara ya fedha saa za kazi kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri siku za kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **14/02/2019** saa **7.00** mchana, ufunguzi wa zabuni utafanyika siku hiyo muda mchache baada ya saa saba.

Waombaji wote au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria siku hiyo ya ufunguzi. Zabuni yoyote ambayo haitasomwa hadharani siku hiyo ya ufunguzi haitashughulikiwa. Bodi ya Zabuni inayo haki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Zabuni kukubali au kukataa ombi lolote la Zabuni la bei ya chini au ya juu. Waombaji wote waliopata na wasiopata watajulishwa matokeo ya maombi yao ya zabuni.

Wenu katika Ujenzi wa Taifa,



Dr. Gabriel Chitupila

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
**HALMASHAURI YA WILAYA,
KIBONDO**



Nakala:

“ Katibu Tawala (M),
S.L.P. 125,
KIGOMA

“ Katibu Tawala (W),
S.L.P 3,
KIBONDO

“ Mbao zote za Matangazo.